



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA KUREKEBISHA SHERIA TANZANIA**



TAARIFA KWA UMMA

Dodoma 3 Agosti 2025

Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais anayeshughulikia masuala ya Muungano, Bw. Abdala Mitawi, ametembelea banda la Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania (LRCT) katika viwanja vya Nzuguni, jijini Dodoma, ambako Maonesho ya Kilimo ya Nanenane yanaendelea.

Bw. Mitawi alieleza kufurahishwa na kazi inayofanywa na Tume hiyo, hususan jitihada zake za kupitia, kupendekeza, na kuandaa marekebisho ya sheria mbalimbali ili ziendane na wakati, na kutatua changamoto za kiutendaji, kijamii na kiuchumi.

“Nimeridhishwa na kazi mnayoifanya, hususan katika kuhakikisha kuwa sheria zinazotumika nchini zinaandana na mabadiliko ya kijamii na kiteknolojia, alisema Bw. Mitawi.

Akiwa katika banda hilo, Naibu Katibu Mkuu alipata fursa ya kuangalia machapisho mbalimbali ya kisheria yaliyoandaliwa na Tume, pamoja na kupokea maelezo kuhusu mchakato wa ukusanyaji wa maoni kutoka kwa wananchi kabla ya sheria kurekebishwa.

Tume ya Kurekebisha Sheria ni chombo huru cha Serikali kinachowajibika kwa kuishauri Serikali juu ya mapendekezo ya marekebisho ya sheria ili kuhakikisha zinabaki kuwa sahihi, zenye uwiano, na zinazotekelezeka kwa ufanisi.

Maonesho ya Nanenane mwaka huu yanafanyika kuanzia Agosti 1 hadi 8, yakihusisha taasisi mbalimbali za Serikali, binafsi, na asasi za kiraia, zikiwemo zile zinazojihusisha na sheria, kilimo, elimu, afya, na teknolojia ambapo Tume ya kurekebisha Sheria inashriki katika maonesho hayo ili kutoa elimu ya sheria kwa Umma, kupokea maoni ya mapendekezo ya Sheria na kutoa ushauri wa kisheria.

Bashiri S. Juma
Kitengo cha Mawasiliono Serikalini